

MONITORING LEARNERS PROGRESS

GREDI YA 5, MWAKA: 2021

KISWAHILI: LUGHA

S A S O N
0 0 2

Muda: Saa 1 Dak. 40

SEHEMU 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu amsomee mwanafunzi kifungu hiki kisha amwulize maswali yafuatayo.

Paka yuko jikoni. Amebeba panya mdomoni. Panya huyo ni mweusi. Paka anajificha mvunguni mwa meza. Mama anamwona paka.

- i) Paka yuko wapi?
(Mwanafunzi ajibu)
- ii) Paka amebeba nini mdomoni?
(Mwanafunzi ajibu)
- iii) Panya huyo ni wa rangi gani?
(Mwanafunzi ajibu)
- iv) Paka anajificha wapi?
(Mwanafunzi ajibu)
- v) Nani anamwona paka?
(Mwanafunzi ajibu)

Vigezo vya Kutathminia Kusikiliza na Kuzungumza

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	5	4	3	0 - 2

SEHEMU 2: KUSOMA KWA SAUTI (Alama 5)

Mwanafunzi asome kifungu hiki kwa sauti.

Ilikuwa siku ya Ijumaa tulipokuwa sebuleni tukitazama runinga. Babu alianza kutusimulia jinsi ambavyo mwalimu wao alikuwa akiwaeleza kuhusu umuhimu wa miti. Hata ingawa alikuwa shulenii miaka sitini iliyopita, alikuwa akiyakumbuka vizuri.

Alianza kwa kusema kuwa mwalimu wao alisema kuwa miti huwa ni maskani ya wanyama mbalimbali sanasana nyuni ambao hutengeneza

viota vyao na kutagia mayai humo. Aliendelea kutuambia kuwa wanyama wengine wanaotegemea miti kama makazi ni wanyamapori kama vile simba, chui, pundamilia na wengine.

Vigezo vya Kutathminia - Kusoma

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Maneno yaliyosomwa katika dakika moja	60 na zaidi	41 - 60	21 - 40	0 - 20

SEHEMU 3: UFAHAMU (Alama 5).

Mwanafunzi asome kifungu hiki na kujibu maswali.

(a)

NDOTO YA AMINA

Babu alimnunulia Amina godoro na foronya. Usiku alipolala aliota ndoto. Aliota kuwa alikuwa msichana mkubwa. Alikuwa akifanya kazi ya ualimu. Baada ya miaka miwili aliachä ualimu akawa mkulima. Aliuza mazao akapata shilingi laki tatu. Alipokuwa akipeleka pesa zake benkini, aliamka kutoka usingizini.

- i) Nani alimnunulia Amina godoro? _____
- ii) Aliota ndoto wakati gani? _____
- iii) Mara ya kwanza alikuwa akifanya kazi gani? _____
- iv) Baada ya miaka miwili alianza kufanya kazi gani? _____
- v) Alikuwa akipeleka pesa zake wapi? _____

(b)

MWALIMU BIDII

Mwalimu Bidii ni mwalimu wa Kiswahili. Anafundisha katika shule ya msingi ya Hekima. Kila siku yeye hutukumbusha kuwa tuwe watoto safi. Kuna siku alituletea ndizi. Tulifurahia mno. Alituahidi kuwa atatupeleka jijini Mombasa.

- i) Mwalimu Bidii hufundisha somo gani? _____
- ii) Mwalimu Bidii hufundisha katika shule gani? _____

- iii) Mwalimu Bidii huwahimiza wanafunzi kuwa watoto _____
- iv) Mwalimu aliwaletea nini? _____
- v) Mwalimu aliwaahidi kuwa atawapeleka wapi? _____

Vigezo vya Kutathminia - Ufahamu

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	5	4	3	0 - 2

SEHEMU 4: SARUFI

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. jiwe - _____
2. embe - _____
3. mwiko - _____
4. soko - _____
5. fimbo - _____

Andika sentensi kwa wingi.

6. Kiatu chake kimeraruka.

7. Mtoto yule anakula tunda.

8. Goti lake limeumia.

9. Kioo hiki kilivunjika jana.

10. Meza hii ni ya mwanafunzi.

Andika akisami kwa maneno.

11. $\frac{1}{6}$ - _____
12. $\frac{1}{4}$ - _____
13. $\frac{1}{2}$ - _____
14. $\frac{1}{3}$ - _____
15. $\frac{1}{5}$ - _____

Geuza maneno yafuatayo katika hali ya ukubwa.

16. Mto - _____
17. Mtu - _____
18. Mke - _____
19. Mti - _____
20. Mji - _____

Vigezo vya Kutathminia - Sarufi

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	19 - 20	13 - 18	7 - 12	0 - 6

SEHEMU 4: KUANDIKA
INSHA

Andika insha juu ya:

NYUMBANI KWETU

Vigezo vya Kutathminia - Kuandika

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	10	7 - 9	4 - 6	0 - 3